HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 014 | JANUARI - MACHI, 2024

# DKT. IMMACULATE SWARE SEMESI MKURUGENZI MKUU NEMC




Ndani:

- VIWANDA ENDELEVU, MAZINGIRA SAFI NA SALAMA NI KICHOCHEO CHA UCHUMI IMARA
- WAZIRI JAFO AIPONGEZA WIZARA YA ELIMU KWA UTEKELEZAJI WA AGIZO LA KATAZO LA MATUMIZI YA KUNI NA MKAA
- NEMC YAKUTANA NA WADAU KUJADILI NAMNA BORA YA KUDHIBITI UCHAFUZI WA MAZINGIRA - FUKWE YA DENGUE

# YALIYOMO


03 DKT. IMMACULATE SWARE SEMESI MKURUGENZI MKUU NEMC

04 MASHIRIKIANO KATI YA NEMC NA CSE

05 DKT JAFO AWATAKA WAWEKEZAJI KUZINGATIA UFANYAJI WA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KABLA YA UENDELEZAJI WA MRADI

06 NEMC KWA KUSHIRIKIANA NA KITUO CHA SAYANSI NA MANZINGIRA INDIA (CSE,INDIA) YATOA MAFUNZO YA UKAGUZI WA MAZINGIRA.

07 VIWANDA ENDELEVU, MAZINGIRA SAFI NA SALAMA NI KICHOCHEO CHA UCHUMI IMARA

08 WAZIRI JAFO AIPONGEZA WIZARA YA ELIMU KWA UTEKELEZAJI WA AGIZO LA KATAZO LA MATUMIZI YA KUNI NA MKAA

09 UNEP YAOMBWA KUENDELEA KUTOA KIPAUMBELE KWA SERIKALI YA TANZANIA KUPATA FEDHA KWA AJILI YA MIRADI YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

10 DKT. SEMESI ATEMBELEA MRADI WA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI - KONGWA

11 NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA SITA WA BARAZA LA MAZINGIRA LA UMOJA WA MATAIFA (UNEA6) - JIJINI NAIROBI

12 NEMC YATOA ELIMU YA UDHIBITI WA MATUMIZI YA ZEBAKI KATIKA KONGAMANO LA WANAWAKE WACHIMBAJI WADOGO WA MADINI - GEITA

13 NEMC YAZITAKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KOTE NCHINI KUONA FURSA ZILIZOPO KATIKA TAKA NGUMU


14 NEMC YATOA ELIMU YA ATHARI YA UCHAFUZI WA MAZINGIRA NA UCHUMI WA BULUU KWA VIONGOZI WA JIMBO LA ILALA

15 NEMC KWA KUSHIRIKIANA NA KAMISHENI YA BONDE LA ZIWA VICTORIA (LVBC) NA KITUO CHA SAYANSI NA MAZINGIRA (CSE) INDIA YAJADILI UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA KWA ZIWA VICTORIA

16 NEMC YAKUTANA NA WADAU KUJADILI NAMNA BORA YA KUDHIBITI UCHAFUZI WA MAZINGIRA - FUKWE YA DENGUE

17 TANI 2 ZA TAKA ZA MAJUMBANI ZAKUSANYWA NA WANAWAKE WA NEMC ENEO LA MIKOKO KIGAMBONI

18 KAULI YA MAZINGIRA

## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
**Dkt. Menan Jangu**

**Mhariri Mkuu:**
**Irene John**

**Wachangiaji:**
Dalia Charles
Dkt. Rose Mtui
Martha Kawishe
Tajiri Kihemba
Nana Elias
Boniphace Kyaruzi

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# DKT. IMMACULATE SWARE SEMESI MKURUGENZI MKUU NEMC




*Aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu NEMC Dkt. Menan Jangu (kushoto) akabidhi rasmi ofisi kwa Mkrurugenzi Mkuu Mteule wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, 9 Januari 2024, jijini Dodoma.*

Aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Menan Jangu amekabidhi ofisi rasmi kwa Mkurugenzi Mkuu mteule Dkt. Immaculate Sware Semesi kufuatia uteuzi uliofanywa mnamo tarehe 05 Januari 2024 na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hiyo baada ya aliyekuwepo, Dkt. Samwel G. Mafwenga kumaliza muda wake.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo yaliyofanyika tarehe 09 Januari 2024 katika Ofisi za Makao Makuu yaliyopo Dodoma Dkt. Immaculate Sware alimshukuru aliyekua Kaimu Mkurugenzi Mkuu kwa ushirikiano aliompatia wakati wote tangu kustaafu kwa Mkurugenzi aliyekuwepo hadi mabadiliko yalipofanyika mnamo tarehe 05 Januari 2024.

Alisema jukumu kubwa lililo mbele yake katika Baraza la Mazingira ni kuhakikisha maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuitaka Tanzania yenye maendeleo endelevu ya mazingira kwa Usimamizi na Uhifadhi wake kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake yanatekelezwa kwa weledi na misingi imara ikiwa ni pamoja na kutafuta fursa wezeshi za kimazingira katika kuijenga Tanzania ya kijani.

Dkt. Sware alisema kuwa kwa kufanya hivyo kutasaidia kukabiliana na changmoto nyingi za kimazingira kwani azma yake ni kuhakikisha Dira ya Baraza ya kuwa mamlaka ya Kimataifa ya Usimamizi wa Mazingira inayohakikisha mazingira safi, salama na yenye afya kwa watu wa Tanzania inatekelezeka.

Alifafanua kuwa katika uongzi wake ni matarajio yake kuliona Baraza lenye kukuza usimamizi wa Mazingira nchini Tanzania kupitia uratibu, uwezeshaji, uhamasishaji,



*Mkurugenzi Mkuu NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejiment ya Baraza mara baada ya makabidhiano ya ofisi yaliyofanyika katika Ofisi za NEMC Makao Makuu Dodoma.*

utekelezaji, tathmini, ufuatiliaji na utafiti ili kuleta maendeleo endelevu ya Mazingira nchini.

Aidha Mkurugenzi Mkuu Dkt. Sware aliainisha maadili ya msingi atakayosimamia kipindi chote cha uongozi wake ili kufikia malengo chanya yanayogusa dira ya Taifa ya 2025 katika sekta ya Mazingira kuwa ni; uwazi na uwajibikaji, utaalamu na ubora, ushirikiano, utawala bora, usawa, uadilifu na ushiriki wa wadau.

Mkurugenzi Mkuu Mteule alisisitiza mashirikiano na vyombo vya habari, kwani ndio wadau pekee watakaoweza kulifanya Baraza kutambulika kwa majukumu yake ya utoaji elimu kwa wadau pamoja na umuhimu wa uimarishaji wa rasilimali watu kwani ndio nguzo na mhimili wa utekelezaji wa majukumu katika sekta yeyote ile ya kazi.

Aliwataka watendaji wa Baraza kushirikiana kwa pamoja katika utekelezaji wa majukumu ya Kimazingira ili kufikia malengo mahususi ya kuiona Tanzania yenye mazingira safi katika nyanja zote. Pia aliahidi kuimarisha ushirikiano kwa viongozi wa Vyama na Serikali, Taasisi za Umma na Binafsi, sekta za Viwanda na Biashara, Mashirika ya Umma na Binafsi, wadau wa mazingira pamoja na Taasisi wezeshi katika kusukuma gurudumu la maendeleo endelevu ya mazingira na Taifa.

# MASHIRIKIANO KATI YA NEMC NA KITUO CHA SAYANSI NA MAZINGIRA CSE, INDIA

## Warsha ya kujengeana uwezo wa kutathmini matumizi ya nyenzo za ukusanyaji taarifa za taka ngumu nchini




*Wataalamu wa NEMC wakiwa katika picha ya pamoja na Maafisa Mazingira wa Mikoa, Miji na Majiji baada ya Warsha ya kujengeana uwezo wa kutathmini matumizi ya nyenzo za ukusanyaji taarifa za taka ngumu nchini.*

### UTANGULIZI

NEMC kama chombo chenye dhamana ya mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake, imekuwa ikishirikiana na kituo cha Sayansi na Mazingira cha India (CSE) kwa takribani miaka saba katika nyanja ya elimu ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu na kujengeana uwezo wa usimamizi wa mazingira. Makubaliano kati ya taasisi hizi mbili yalisainiwa rasmi mnamo Januari, 2023 na yalilenga katika nyanja za utafiti wa Mazingira, Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), Kaguzi za Mazingira pamoja na Usimamizi wa Taka Ngumu. Aidha, katika dhana nzima ya usimamizi wa taka ngumu, NEMC na CSE kwa pamoja wamekuwa wakiandaa Mikutano na Majukwaa Endelevu ya Ukuaji wa Miji na Majiji (Global Forum of Cities for Circular Economy - GFCCE) yanayoshirikisha wataalamu kutoka ndani na nje ya nchi yenye lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi unaozingatia kutokuwepo kwa taka (zero waste).

Jukwaa Endelevu la Ukuaji wa Miji na Majiji (Global Forum of Cities for Circular Economy) lilianzishwa mnamo Januari, 2022 kwa ajili ya kutoa fursa kwa washiriki kutoka mabara ya Afrika na Asia Jijini Dar es Salaam.

(20) zilizopo Ukanda wa Dunia ya Kusini kuweza kubadilishana uzoefu katika nyanja za Kisera, Kisheria na Kitaaluma ili kuboresha usimamizi wa mazingira na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi. GFCCE inajumuisha nchi 15 za Afrika (Cameroon, Cote d'Ivoire, Ethiopia, Eswatini, Ghana, Kenya, Mozambique, Namibia, Rwanda, Senegal, Afrika Kusini, Tanzania, Uganda, Zambia and Zimbabwe) na 5 za Asia (India, Bangladesh, Bhutan, Nepal na Sri Lanka). Aidha, mashirikiano hayo pia yanahusisha mafunzo ya matumizi ya nyenzo za kidigitali katika kukusanya taarifa zitakazosaidia katika kufanya maamuzi.

Kongamano la awali la GFCCE lilifanyika July, 2022 na kufuatiwa na kongamano la Januari, 2023 nchini lililohusisha wakaguzi wa mazingira, wataalamu elekezi wa mazingira, wamiliki wa viwanda na maafisa mazingira kutoka katika ngazi za Mikoa na Halmashauri. Aidha, mnamo tarehe 5 – 7 Februari, 2024 NEMC na CSE waliandaa Kongamano la 5 (5th GFCCE) lenye lengo la kuwajengea uwezo maafisa mazingira wa Mikoa, Miji na Majiji nchini juu ya matumizi ya nyenzo za kidigitali (A Solid Waste Management Scheme (SWM) Toolkit)) katika kuboresha usimamizi wa taka ngumu. Mafunzo hayo yalifanyika katika hoteli ya New Africa iliyopo jijini Dar es Salaam.

### UMUHIMU WA NYENZO ZA KIDIGITALI

Nyenzo za kidigitali ni muhimu katika kukusanya taarifa ambazo zitasaidia kuwa na maamuzi na mipango dhabiti ya usimamizi wa taka nchini. Aidha, changamoto kubwa inayozikumba Halmashauri nyingi nchini ni ukosefu wa takwimu sahihi juu ya taka zinazozalishwa, kuratibiwa na kuteketezwa. Changamoto hii inaweza kutatuliwa kwa kuwekeza kwenye teknolojia sahihi na rahisi kwa matumizi.





# DKT. JAFO AWATAKA WAWEKEZAJI KUZINGATIA UFANYAJI WA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KABLA YA UENDELEZAJI WA MRADI




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo (mwenye suti yeusi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Zuber Homera (katikati kushoto) pamoja na wananchi na wawekezaji walipozuru mto Zira kujiridhisha na changamoto za kimazingira zilizopo.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo amewataka wawekezaji kote nchini kuzingatia umuhimu wa ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya uendelezaji wowote wa mradi ili kunusuru afya ya mazingira.

Mhe. Waziri alitoa kauli hiyo alipozuru eneo la Mto Zira lililopo Kata ya Ifumbo, Wilaya ya Chunya Mkoa wa Mbeya ili kujiridhisha na changamoto za kimazingira zinazotokana na uchimbaji wa madini unaofanywa na mwekezaji wa Kampuni ya ***"G & I Tech Trading Company Limited".***

Dkt. Jafo alisema uzingatiaji wa ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira unasaidia kuainisha changamoto za kimazingira zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji na kutafuta mbinu mbadala za kuzuia ili kunusuru Mazingira na uhai wa binadamu.

Aliagiza Mamlaka husika kuhakikisha mwekezaji huyo anafanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kutekeleza masharti yote atakayowekewa ili kutosababisha uharibifu wa mazingira na kuathiri mazingira kwa kizazi cha sasa na baadae.

Aliongeza kuwa Serikali ya Mhe. Samia Suluhu Hassan inasisitiza uwekezaji unaozingatia Sheria ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake ili kuepukana na uharibifu wa mazingira unaoweza kutokea.



*Muonekano wa  Mto Zira baada ya uchimbaji wa madini unaofanywa na muwekezaji huko Chunya, Mkoani Mbeya*

# NEMC KWA KUSHIRIKIANA NA KITUO CHA SAYANSI NA MAZINGIRA INDIA (CSE, India) YATOA MAFUNZO YA UKAGUZI WA MAZINGIRA



***NEMC na Taasisi ya Sayansi ya Mazingira India (CSE) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kuzindua toleo la Kitabu cha Tathmini ya Mchakato wa Ukaguzi wa Mazingira kwa Nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara.***

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Kituo cha Sayansi na Mazingira cha nchini India waliendesha warsha ya mafunzo ya siku tatu yenye lengo la kubadilishana uzoefu katika kufanya kaguzi za mazingira (Environmental Audit Study Systems). Mafunzo hayo yalifanyika katika Hoteli ya Four Ponts by Sheraton, New Africa Hotel, Dar es Salaam kuanzia tarehe 24 had 26, Januari, 2024. Jumla ya washiriki 15 kutoka Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara walishiriki mafunzo hayo.

Aidha, warsha hiyo ilitanguliwa na uzinduzi wa taarifa ya Tathmini ya Mfumo wa Ukaguzi wa Mazingira kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Katika taarifa hiyo, ilibainika kuwa ripoti nyingi za kaguzi za mazingira zinazoandaliwa hazina taarifa za kutosha (data) kuweza kusaidia kufanya maamuzi sahihi. Kwa mfano, ripoti za miradi ya viwanda iliyokaguliwa zilionekana kukosa takwimu za kiwango cha uzalishaji, aina za nishati zinazotumika na wingi wake, viwango vya matumizi ya rasilimali maji na majitaka yanayozalishwa, aina pamoja na viwango vya taka ngumu zinazozalishwa. Aidha, ripoti hizo hazikuainisha takwimu zilizokusanywa kipindi cha nyuma ambazo zinaweza kuchambuliwa na kusaidia katika kuainisha mapendekezo.

Pia, changamoto nyingine kubwa iliyoainishwa katika ripoti hiyo ni kukosekana kwa mifumo dhabiti ya usimamizi wa Sheria ili kutoruhusu viwanda vinavyochafua mazingira kuendelea kufanya kazi. Katika ripoti hiyo, mapendekezo kadhaa yalitolewa ambayo ni pamoja na:-

i. Mamlaka za usimamizi wa mazingira ziandae mwongozo wa ukaguzi unaoainisha miradi inayostahili kufanyiwa ukaguzi wa mazingira pamoja na vigezo vya kuzingatia wakati wa ukaguzi. Hii itaepusha kujumuisha miradi isiyochafua mazingira katika kundi la miradi inayohitaji kufanyiwa kaguzi za mazingira.

ii. Mamlaka ziandae miongozo ya kisekta ya kaguzi za mazingira kwa viwanda, miradi ya kilimo, uchimbaji n.k. Hii itasaidia kuweka mipaka ya kiutendaji na kuboresha uandishi wa ripoti.

iii. Kuwepo na *program* maalumu ya kuwajengea uwezo watalaam elekezi na wakaguzi wa mazingira. Hii itasaidia kuainisha aina ya taarifa zinazohitajika kwenye ripoti na umuhimu wa kujumuisha taarifa hizo katika ripoti za kaguzi. Aidha, maafisa wanaofanya mapitio ya taarifa za kaguzi wataweza kujifunza namna bora ya kutoa mapendekezo yenye tija.

Kaguzi za mazingira hufanyika kwa mujibu wa Sheria, Miongozo na Kanuni; na hulenga kutathmini uzingatiaji wa viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, kaguzi za mazingira hufanyika kwa miradi yote ya kiuchumi na kijamii na huusisha tathmini ya kina ya uendeshaji, usimamizi na utendaji kazi wa mifumo ya mradi husika ili kujiridhisha na athari zinazoweza kutokana na shughuli hizo pamoja na kutoa mapendekezo.



***Washiriki wakifuatilia Mafunzo ya Ukaguzi wa Mazingira, Januari 24-26, 2024***

# VIWANDA ENDELEVU, MAZINGIRA SAFI NA SALAMA NI KICHOCHEO CHA UCHUMI IMARA







Shughuli za viwanda nchini Tanzania ni miongoni mwa sekta kubwa inayochangia pato la Taifa, ajira kwa vijana na kupelekea uchumi wa nchi kukua kwa kasi.. Sekta hii imekua kutokana na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo nchini mfano viwanda vya nguo, ngozi, saruji, uchakataji wa chuma na plastiki.

Viwanda vinachochea mageuzi ya kimfumo kwenye jamii hasa katika sekta za kilimo na madini. Hivyo kuwa na viwanda vingi nchini inachangia uwepo wa bidhaa ndani ya nchi na kupanua wigo wa upatikanaji wa bidhaa na huduma. Hii itapanua wigo katika chaguzi na mahitaji ya watu.

Uchumi wa Nchi hutegemea kwa kiasi kikubwa na kupatikana kwa viwanda ambavyo hutoa ajira kwa wananchi na mapato kwa ajili ya maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Kwa mfano, kilimo cha pamba kinachochea viwanda kupata malighafi kwa ajili ya kutengeneza nguo, inachangia kuongeza ajira kwa wananchi wanaojihusisha na kilimo pamoja na uzalishaji viwandani. Hivyo hatuwezi kutenganisha viwanda na kilimo.

Ili kuweza kufikia lengo la kufanya uzalishaji ulio thabiti kwa kizazi kilichopo na kijacho ni muhimu kutunza mazingira. Viwanda vinachangia uchumi wa Nchi kukua na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto nyingi kwa wamiliki wa viwanda kutokuzingatia Sheria za kutunza na kuhifadhi Mazingira.

Kuzingatia utunzaji wa mazingira ni jambo la msingi ili kukuza uchumi wa nchi kwani mazingira yakiharibika na uchumi wa Taifa nao utakuwa umeharibika na kusababisha Taifa la watu wenye changamoto yakiwemo maradhi.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limekuwa kinara katika kuhakikisha mazingira yanakuwa safi na salama ili kuwezesha wananchi pamoja na wawekezaji kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake. Hii ni kulifanya Taifa kuwa na viwanda endelevu, uchumi imara na mazingira safi na salama kwa maendeleo ya nchi.

Licha ya kuwepo kwa Sheria ya usimamizi wa Mazingira, uchafuzi wa mazingira bado unaendelea hasa unaohusisha taka za majumbani na hospitalini zikiwemo mifuko ya plastiki, mabaki ya vyakula na taka hatarishi kama vyuma chakavu, taka za hospital n.k.

Taka nyingine ni majitaka yaliyochanganyika na kemikali au vinyesi kutoka viwandani yanayotiririshwa kuelekea kwenye vyanzo vya maji na mifereji. Hili ni tatizo kubwa nchini licha ya viwanda kutozwa faini kubwa kutokana na tatizo hili. Hata hivyo bado changamoto hio imeendelea kuwa mwiba japo kumekuwa na jitihada za makusudi zinazofanywa na Baraza katika kuhakikisha kuwa Sheria ya Mazingira inazingatiwa na kutekelezwa.

Baraza limekuwa likikagua mazingira viwandani ili kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa katika viwanda hivyo unafanyika bila ya kuathiri mazingira. Changamoto za uchafuzi wa mazingira zipo nyingi kwani malalamiko ni mengi kutoka kwa wananchi juu ya utiririshaji maji machafu yenye kemikali katika mifereji kabla ya kutibiwa.

Suala hili limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka viwanda kwani wamekua wakipata athari za kiafya kutokana na maji hayo kuingia kwenye vyanzo vya maji pamoja na harufu kali ya maji taka yanayotuama kwenye mifereji madimbwi na mitaro.

Licha ya jitihada nyingi zinazofanywa na Serikali za udhibiti wa uharibifu wa mazingira kwa kutoza faini na kusitisha shughuli zinazofanywa na viwanda, bado haijasaidia kupunguza tatizo husika.

Hivyo juhudi za kutoa elimu zinapaswa kuongezwa hasa katika njia bora za utiririshaji maji taka kutoka kwenye viwanda. Kuna namna mbalimbali za kusimamia maji taka kwa kuchagua njia ya kutibu maji kwa mfumo unaofaa na kupunguza athari za uchafuzi wa mazingira na madhara ya kiafya kwa wananchi. Hivyo, mifumo ya kutumia kemikali kutibu maji, kuweka mitambo maalum ya kukusanya maji taka,na ufuatiliaji wa pamoja na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria, itasaidia kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na badae kwani Mazingira yetu ni Uhai wetu.

# WAZIRI JAFO AIPONGEZA WIZARA YA ELIMU KWA UTEKELEZAJI WA AGIZO LA KATAZO LA MATUMIZI YA KUNI NA MKAA



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiongea na wandishi wa habari wakati wa utoaji taarifa ya utekelezaji wa agizo la katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa Wizara na Taasisi zake.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ameipongeza Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa kuwa kinara wa utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais juu ya katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi za umma zinazoandaa na kulisha watu zaidi ya mia moja (100) kwa siku, kuanzia Januari, 2024.

Pongezi hizo zilitolewa na Mhe. Jafo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari februari 20, 2024 katika ofisi za Makao Makuu ya NEMC Jijini Dodoma na kutoa taarifa ya utekelezaji wa maelekezo ya Serikali yahusuyo usitishaji wa matumizi ya kuni na mkaa kwa Taasisi za Umma na kubainisha Wizara hiyo kupitia taasisi zake kuwa imetekeleza kwa zaidi ya asilimia 85.

Alisema lengo la maelekezo hayo ni kupunguza madhara ya kiafya na mazingira yanayosababishwa na kukithiri kwa matumizi ya kuni na mkaa katika jamii zetu na ukataji wa miti kwa ajili ya nishati ya kupikia.

Dkt. Jafo alisisitiza kuwa katazo hilo haliwahusu watumiaji katika ngazi ya kaya na watumiaji wadogo bali limeanza kwa watumiaji wakubwa.

> **"Katika utekelezaji wa agizo hilii, napenda kuipongeza Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa kuwa kinara kwa Taasisi zake nyingi kutekeleza agizo hili la Serikali kwa zaidi ya asilimia 85. Taasisi nyingine zinapaswa kuiga mfano mzuri uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi zake."**
>
> Alisema Waziri Jafo.

Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waanze kutumia nishati safi ya Kupikia.

"Kama nilivyosema, awali, katazo hili linazihusu Taasisi kubwa, Taasisi hizo ziko chini ya TAMISEMI, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, jinsia na makundi maalumu, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi" Amesema Dkt Jafo.

Mhe. Jafo alisema Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 inahimiza umuhimu wa kulinda na kuhifadhi Mazingira ikiwemo rasilimali za misitu, hivyo ili kufikia lengo hilo, sera inahamasisha matumizi ya nishati mbadala ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza ukataji miti

Katika hatua nyingine Waziri Jafo alisema kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta ipo kwenye maandalizi ya kuunda timu ya Wataalam itakayoweza kutembelea taasisi husika ili kufuatilia hatua zinazoendelea katika utekelezaji wa katazo hilo na kutoa ushauri wa kitaalam.

Itakumbukwa kuwa tarehe 01 Novemba, 2022, Jijini Dar es Salaam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ya kusitisha matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya mia moja (100) kwa siku, ifikapo Januari, 2024. Lengo la maelekezo hayo ni kupunguza madhara ya kiafya na mazingira yanayosababishwa na kukithiri kwa matumizi ya kuni na mkaa katika jamii zetu.

# UNEP YAOMBWA KUENDELEA KUTOA KIPAUMBELE KWA SERIKALI YA TANZANIA KUPATA FEDHA KWA AJILI YA MIRADI YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA



Shirika la Usimamizi wa Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) limeombwa kuendelea kutoa kipaumbele kwa Serikali ya Tanzania kupata fedha za utekelezaji miradi ya kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Ombi hilo lilitolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais(Muungano na Mazingira) Bi. Mary Maganga katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Kemilembe Mutasa wakati wa kikao cha Uratibu wa Tathimini ya Miradi ya Mazingira inayosimamiwa na UNEP nchini.

Bi. Kemilembe alisema UNEP imeendelea kuwa mshirika wa maendeleo na Tanzania kupitia kufadhili miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Hifadhi ya Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa, Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai (SLR) na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini (EBBAR).

Bi. Maganga alisema kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika miradi hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imewasilisha maandiko ya miradi mipya ya vipaumbele inayohitaji fedha zaidi kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za Kimataifa za mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Tunaishukuru shirika la UNEP kwa ushirikiano wa karibu na Tanzania katika jitihada za pamoja za kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha jamii yetu na dunia kwa ujumla inaendelea kubaki salama," alisema Bi. Maganga.

Aliongeza kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za asili ikiwemo misitu, mito, maziwa na bahari ambapo maeneo katika rasilimali hizi yametengwa kwa ajili ya manufaa ya wananchi na dunia kwa ujumla na kupitia mikataba na itifaki za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Alisema kutokana na umuhimu wa rasilimali hizo, Tanzania imeendelea kupiga hatua kubwa katika kusimamia na kutekeleza miradi ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha ushirikiano na wadau pamoja na mashirika ya maendeleo ili kufikia malengo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Bi. Maganga aliongeza kwa kusema kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais pia imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuhuisha Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.



# DKT. SEMESI ATEMBELEA MRADI WA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI - KONGWA



*Mkurugenzi Mkuu NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi (mwenye pinki katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wananchi wanufaika na mradi wa kuhimili mabadiliko ya Tabianchi Wilaya ya Kongwa alipozuru eneo hilo.*

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi ametembelea mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi uliopo Wilayani Kongwa kwa lengo la kujionea hatua.

za utekelezaji wa mradi huo, ikiwa ni pamoja na kubaini changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wake na kushauri namna bora ya kuenenda katika ukamilishaji ili kuleta tija na ufanisi kwa maendeleo endelevu ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Katika ziara yake, Dkt Sware alikutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Dkt. Omary A. Nkullo, pamoja na wataalamu wa mazingira kutoka NEMC, TAMISEMI na Shirika la Foundation for Energy, Climate and Environment (FECEO katika kikao cha pamoja cha mrejesho wa ziara ya wataalamu ya ukaguzi wa miradi ya kimazingira inayotekelezwa katika Kata za Ugogoni na Mtanana, Wilaya ya Kongwa, na kushauri namna bora ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Kadhalika Dkt. Sware pia alipata fursa ya kuzindua zoezi la upandaji miti eneo la mradi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa malengo kusudiwa ya mradi yenye mrengo unaotoa chachu ya kutunza na kuhifadhi mazingira katika maeneo yote ya miradi ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira.

# NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA SITA WA BARAZA LA MAZINGIRA LA UMOJA WA MATAIFA (UNEA6) - JIJINI NAIROBI



*Waziri wa Nchi Oisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo (katikati), akiwa katika picha ya Pamoja na washiriki wa mkutano wa (UNEA 6) kutoka Tanzania mara baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mkutano huo.*

Baraza la Mazingira (NEMC) lilishiriki Mkutano wa sita wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA 6) uliofunguliwa februari 26 2024 katika Makao Makuu ya Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) jijini Nairobi.

Lengo kuu la Mkutano huo lilikuwa ni kuandaa Sera kuhusu Mazingira, ambayo inalenga kurejesha maelewano kati ya binadamu na Mazingira, ili kuboresha maisha ya watu wanaokabiliwa na changamoto za kimazingira.

Mkutano wa UNEA6 ulikutanisha viongozi kutoka Mataifa mbalimbali duniani, ikiwemo Tanzania kujadili masuala mbalimbali ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi, uharibifu wa bioanuai na uchafuzi wa mazingira.

Tanzania ni miongoni mwa Nchi zinazokabiliwa na athari za mabadiliko ya Tabianchi ambayo husababisha ukame, uhaba wa mvua, mafuriko na vifo kwa wanyama.

Aidha mkutano huu ulitoa fursa kwa Serikali za Nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa, wanaharakati wa mazingira, wanasayansi, Sekta binafsi, Taasisi za fedha na Asasi za Kiraia kupaza sauti na kuhusishwa katika kutunga Sera ya Ulimwengu mzima kuhusu Mazingira.

Kaulimbiu ya Mkutano wa UNEA6 kwa mwaka 2024, ni juhudi madhubuti, jumuishi na endelevu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa bioanuai na uchafuzi wa mazingira.

Aidha, Ujumbe wa Tanzania uliambatana na wataalamu kutoka NEMC, Waziri mwenye dhamana ya Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo na wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

# NEMC YATOA ELIMU YA UDHIBITI WA MATUMIZI YA ZEBAKI KATIKA KONGAMANO LA WANAWAKE WACHIMBAJI WADOGO WA MADINI - GEITA

"Kemikali inayotumika na Wachimbaji ambao mitaji yao ni midogo na hasa wanawake ni Zebaki, na hii ni moj moja moja ya kemikali zenye athari kubwa za kiafya na kimazingira. Tumewapa wanawake thamani ya kipekee kwa sababu tabia ya kemikali ya Zebaki yenyewe ni kwamba inabebwa kutoka kiumbe kimoja kwenda kingine kwa hiyo ikiingia kwa mama aliyefika umri wa kushika mimba madhara yake yatahamia kwa mtoto na kusababisha madhara ya kiafya"

Alisema Mhandisi Dkt. Befrina Igulu

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Kemikali ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo (EHPMP) lilitoa elimu ya udhibiti wa matumizi ya kemikali ya zebaki kwa wanawake wachimbaji katika Kongamano la Wanawake Wachimbaji Wadogo Mkoani Geita. Huu ni muendelezo wa Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa kila tarehe 08 ya mwezi Machi kila mwaka.

Baraza liliwakilishwa na Mratibu wa Mradi huo Mhandisi Dkt. Befrina Igulu ambapo alitumia jukwaa hilo kuzungumza na wanawake wanaojishughulisha na uchimbaji wa dhahabu Mkoani Geita na kuelezea nia ya Serikali ya kuwa na mpango wa kupunguza na hatimae kuondoa kabisa matumizi yake katika kuchenjua dhahabu kutokana na kuwa na athari nyingi kiafya na kimazingira.

"Madhara yake ni pamoja na mimba kuharibika, mtoto kuzaliwa na uelewa hafifu jambo ambalo linaharibu ustawi wa jamii kiujumla. Kama Serikali ni nia yetu ya dhati tupunguze na ikiwezekana kuacha kabisa matumizi ya Zebaki" Ameongezea Dkt. Befrina.

Baraza linatekeleza mradi wa kudhibiti matumizi ya kemikali ya Zebaki kufuatia makubaliano ya kidunia ya kuondoa kabisa matumizi ya Zebaki hadi kufikia mwaka 2030 hivyo Serikali imedhamiria kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo ili waanze kutumia njia mbadala za uchenjuaji wa dhahabu.




*Mratibu wa mradi wa kudhibiti matumizi ya kemikali ya Zebaki kutoka NEMC Dkt. Befrina Igulu akifafanua jambo katika kongamano la wanawake wachimbaji wa madini ya dhahabu lililofanyika Mkoani Geita.*

# NEMC YAZITAKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KOTE NCHINI KUONA FURSA ZILIZOPO KATIKA TAKA NGUMU




*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Programu India (CSE) Mr. Atin Biswasi(kulia kwake) pamoja na washriki wa mfunzo ya udhibiti wa taka ngumu mara ya kukamilika kwa mafunzo yaliyofanyika katika ukumbi wa New Africa Dar es salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeyataka Majiji, Halmashauri za Miji na Manispaa kuona na kutambua fursa za ajira zilizopo katika taka ngumu na kuweka mikakati wezeshi ya kufanikisha adhma hiyo ili kutunza Mazingira.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi wakati akifungua mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na NEMC kwa kushirikiana na Kituo cha Sayansi ya Mazingira (CSE) cha nchini India kuhusu udhibiti wa taka ngumu.

Alisema taka ngumu ni fursa wezeshi ya ajira kwa vijana hasa ikitumiwa kutengeneza nishati na bidhaa mbalimbali ili kuyaweka itakayoweka mazingira katika hali ya usafi.

Aliongeza kuwa upo umuhimu wa kukusanya takwimu ya taka zinazozalishwa kwenye maeneo mbalimbali nchini na namna zinavyotunzwa ili ziwe fursa kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali hasa ikizingatiwa kituo Cha Sayansi Cha India (CSE) tayari kimesha andaa mwongozo wa namna ya kuzitumia taka hizo kama rasilimali.

"Taka ngumu kwenye Manispaa zetu Tanzania zinaendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la shughuli za binadamu, kwa hiyo tunapaswa kuangalia namna ya kutumia taka ngumu kuwa fursa na ili kuyaweka mazingira yetu safi," alisema Dkt. Sware.

Naye Mkurugenzi wa Tafiti za Mazingira (NEMC), Dk. Menan Jangu alisema upo umuhimu wa kuboresha mifumo ya udhibiti wa taka ngumu ambazo zimekuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira nchini kwani Serikali kwa kushirikiana na wadau na kituo Cha CSE India tayari wameweka mikakati ya kuhakikisha taka ngumu zinakuwa fursa.

Mkutano huo ulishirikisha maofisa kutoka Manispaa na Majiji kutoka Mikoa sita ikiwemo Dar es salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Tanga kwa lengo la kuwajengea uelewa na kuwapa mikakati ya kusimamia taka ngumu kwenye maeneo yao.

# NEMC YATOA ELIMU YA ATHARI YA UCHAFUZI WA MAZINGIRA NA UCHUMI WA BULUU KWA VIONGOZI WA JIMBO LA ILALA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa elimu ya uchafuzi wa mazingira na Uchumi wa buluu katika mkutano wa viongozi wa jimbo la Ilala ulioandaliwa na Mhe. Abbas Zuberi (Mb.).

Akizungumza katika mkutano huo, Meneja wa Tafiti za Mazingira kutoka NEMC Dkt. Rose Salema Mtui aliyaainisha majukumu ya Baraza kama chombo kinachosimamia Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira mwaka 2004 na Kanuni zake .

Dkt Rose pia alifafanua athari za kimazingira zitokanazo na shughuli za kibinadamu zisizozingatia misingi ya Uhifadhi na Utunzaji wa mazingira na kuitaka jamii hiyo kuepukana nazo.

Alisema uchafuzi wa mazingira ni jambo lililokithiri na linaloleta athari kubwa hasa athari za mabadiliko ya tabianchi hali inayorudisha nyuma maendeleo ya Nchi kutokana na uharibifu wa ikolojia za Bahari, uoto wa asili na kusababisha ukame kwa badhi ya maeneo na kuwataka wananchi hao kuzingatia utunzaji ili kupeukana nazo.



*Meneja wa Tafiti za Mazingira (NEMC) Dkt. Rose Sallema Mtui akifafanua mada ihusuyo athari za uchafuzi wa mazingira na Uchumi wa buluu katika mkutano wa wananchi wa Jimbo la Ilala ulioandaliwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es salaam.*

Kadhalika alieleza umuhimu wa Uchumi wa Buluu kwa jamii na kusisitiza utunzaji wa mazingira kwani uchafuzi wa mazingira utokanao na taka ngumu na kemikali huathiri viumbe wa baharini na baadae kuathiri afya ya binadamu, alisema Dkt. Rose.



*Wananchi wa Jimbo Ilala wakifuatalia mada ya Athari za Uchafuzi wa Mazingira na uchumi wa Buluu inayotolewa na Meneja wa Tafiti za Mazingira kutoka NEMC Dkt. Rose Sallema Mtui.*

# NEMC YAKUTANA NA WADAU KUJADILI NAMNA BORA YA KUDHIBITI UCHAFUZI WA MAZINGIRA - FUKWE YA DENGUE



*Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Dkt. Thobias Mwesiga (Mbele) akiwa na wadau wa Mazingira wa Fukwe ya Dengue kwenye kikao kilichofanyika Ofisi za Baraza Dar es salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limekutana na wawakilishi kutoka DAWASA, Gymkhana Club, Marine Park, Jiji la Dar es salaam na Mkoa kwa lengo la kujadiliana namna bora ya kudhibiti majitaka eneo la fukwe ya Dengue Aghakan Jijini Dar es salaam.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa Baraza Dar es salaam, Kaimu Mkurugenzi wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Dkt. Thobias Mwesiga alisema Baraza kama chombo kinachosimamia Sheria lina wajibu wa kukutana na wadau na kujadiliana namna bora ya kukabiliana na changamoto za Mazingira katika eneo husika ili kwa pamoja kuweza kuyalinda.

Dkt. Thobias alisisitiza kuwa eneo hilo la fukwe ya Dengue limekuwa na changamoto ya kutiririsha maji taka hali inayosababisha kero ya harufu kali kwa wananchi wanaozunguka eneo kutokana na watu wachache wasiokuwa waaminifu kuunganisha kiholela bomba la maji taka kwenye mfumo wa bomba la maji ya mvua lililoelekezwa katika fukwe hizo.

Katika kikao hicho cha wadau wa Mazingira na wataalamu, Baraza limewataka DAWASA na Jiji kudhibiti uchafuzi wa Mazingira katika fukwe na kuondoa kero ya harufu kali kutokana na utiririshaji wa maji.

# NEMC kwa Kushirikiana na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) na Kituo cha Sayansi na Mazingira (CSE) India yajadili Utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira kwa Ziwa Victoria



*Picha ya pamoja kati ya NEMC, CSE India Pamoja na maafisa kutoka Kenya, Tanzania, Burundi, Uganda na Rwanda baada ya kikao kujadiliana kuhusu Utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira kwa Ziwa Victoria.*

Ziwa Victoria ni mojawapo ya vyanzo vya maji vyenye umuhimu mkubwa sana kiikolojia.

Ziwa hili limezungukwa na nchi tatu ambazo ni Tanzania (51%), Uganda (44%) na Kenya (5%). Ziwa hili linahudumia takribani wakazi wapatao milioni 45 ambao wanalitegemea kwa shughuli za uvuvi, kilimo, utalii, viwanda na biashara. Takribani kwa miongo mitano iliyopita, Ziwa hili limekuwa likikumbwa na changamoto mbalimbali ambazo zinatokana na shughuli za kibinadamu.

Kutokana na hali hiyo, mnamo mwaka 2020, NEMC kwa kushirikiana na CSE walianza kufanya uchambuzi wa kina (situational analysis) ili kuainisha changamoto zilizopo na kuangalia namna bora ya kuzitatua. Uchambuzi huo wa awali ulihusisha uchambuzi wa ripoti, machapisho ya kisayansi, taarifa za ufuatiliaji na makala zilizoandaliwa na kuchapishwa kwenye ripoti iliyotambulika kwa jina la 'Discussion Paper – Tanzania; Development of Environmental Management Stratergy Towards Sustaining Ecological Intergrity of Lake Victoria, 2022'. Katika uchambuzi huo, Jiji la Mwanza lilionekana kuwa ndiyo kitovu cha uchafuzi wa mazingira kwa Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania. Uchafuzi huo unatokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo majitaka kutoka majumbani na viwandani ambayo hutiririshwa kupitia mito inayoingiza maji ziwani ikiwemo Mto Mirongo na Nyashishi. Aidha, taka ngumu zinazozalishwa na kutohifadhiwa vizuri na hivyo kupelekea kuzagaa hadi maeneo yaliyo jirani na Ziwa.



*Wadau wa mazingira wa Ziwa Victoria kutoka Tanzania, Uganda, Rwanda, Kenya na Mashirika ya Kikanda wakiwa katika kikao kuadiliana Utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira kwa Ziwa Victoria kilichoandaliwa na NEMC kwa kushirikiana na CSE India*

Katika kukabiliana na hali hiyo, NEMC na CSE waliandaa mpango kazi wa utatuzi wa changamoto hizo 'Roadmap for Management of Water Quality in Mwanza City, Tanzania 2023'. Mpango huo umeainisha hatua mbalimbali zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza uchafuzi wa ziwa Victoria. Hatua hizo ni pamoja na mkakati wa kufanya Jiji la Mwanza kuwa taka-sifuri, urejelezwaji wa ardhi oevu ili kuzuia uchafu unaoingia ziwani, kutengeneza mifumo bora ya kutibu maji taka yanayotoka majumbani, kupima ubora wa maji mara kwa mara na kufanya ufuatiliaji.

Warsha hiyo ilihudhuriwa na wadau wa Nchi za Maziwa Makuu zilizopakana na Ziwa Victoria ambazo ni Mamlaka za Mazingira za Rwanda, Kenya, Uganda na Wizara ya Mazingira, Kilimo na Ufugaji kutoka Burundi. Kwa upande wa Tanzania wawakilishi walitoka NEMC, Mamlaka ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBWB), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Jiji la Mwanza, pamoja na Maafisa Mazingira kutoka mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu na Mara. Aidha, wataalamu kutoka kamisheni ya bonde la Ziwa Victoria (LVBC) pia walishiriki.

Wajumbe walikubaliana kuwa, mashirikiano ni muhimu katika kufanikisha mikakati ya kusimamia mazingira kwa Ziwa Victoria. Aidha, mojawapo ya mambo waliyokubaliana ni pamoja na kuandaliwa kwa protokali ya kikanda ya kushirikishana taarifa (East Africa Protocol on Data Sharing).

# TANI 2 ZA TAKA ZA MAJUMBANI ZAKUSANYWA NA WANAWAKE WA NEMC ENEO LA MIKOKO KIGAMBONI




*Meneja wa Tafiti za mazingira (NEMC), Dkt. Rose Mtui (katikati) akifafanua jambo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu NEMC mara baada ya kukamilika kwa zoezi la kusafisha fukwe iliyopo Kigamboni katika kuenzi siku ya wanawake duniani.*

Tani mbili (2) za taka za majumbani zilizohusisha taulo za watoto, chupa za plastiki, mabati, mabox na mifuko ya plastiki zimekusanywa na wanawake watumishi wa NEMC eneo la Mikoko lililopo Mtaa wa Kibugumo, Kata ya Mji Mwema Wilaya ya Kigamboni katika zoezi la usafi lililofanywa na wanawake hao ili kuenzi kaulimbiu ya mwaka 2024 isemayo " Wekeza kwa wanawake kuharakisha maendeleo ya Taifa".

Akizungumza katika zoezi hilo lililohusisha wadau wa mazingira kutoka Hudefo, Teemo, Manispaa ya Kigamboni, BMU na Silk Kot meneja wa Tafiti za Mazingira kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Rose Salema Mtui alisema uchafuzi wa fukwe na uharibifu wa mikoko na matumbawe na kupoteza uwezo wa kuchuja taka sumu kabla ya kuingia baharini. Hali hii huathiri ustawi wa viumbe baharini, kuharibu mazalia, makuzi na malisho yao unaotokana na uchafuzi wa maji, hali ya hewa na mandhari ya eneo husika.

Dkt. Rose aliwataka wananchi kutambua fursa iliyopo katika kuzitenga taka kuanzia majumbani ili kuepuka utupaji holela katika maeneo yasiyo rasmi pamoja na fukwe hali inayosababisha uharibifu wa Mazingira na viumbe wa majini na mifumo ikolojia.

Naye Kaimu Meneja Kanda ya Mashariki Kusini Bi. Lilian Kapakala alipozungumza alikemea vikali wakandarasi bubu wanaochafua fukwe kwa kutupa taka za majumbani hali inayopelekea uharibifu wa mazingira.


Katika hatua nyingine wanawake wa NEMC na wadau mbalimbali wa mazingira walipanda miche 100 ya mikoko ili kulinda kingo za bahari na kutunza mazingira.



*Rundo la takataka lililokusanywa na wanawake wa NEMC na wadau mbalimbali wa mazingira eneo la Mikoko Kigamboni mara baada ya kusafisha eneo la Mikoko Kigamboni.*

# Kauli ya Mazingira Yetu

## KAULI YA MAZINGIRA YETU



"Uharibifu wa mazingira kutokana na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali zinazounda mifumo ya ikolojia kama misitu, hupelekea mifumo kutokuwa endelevu kwa sababu hushindwa kuhimili athari za uharibifu wa mazingira kama mabadiliko ya hali ya hewa. Tutunze mazingira ili mifumo ikolojia

**TUNZA MAZINGIRA**

## KAULI YA MAZINGIRA YETU



"Mifumo ya ikolojia ina umuhimu katika mazingira kwa sababu inatoa huduma muhimu katika maisha ya viumbe hai akiwemo binadamu kwani hupata chakula, maji, dawa na hewa safi ya oksijeni, husaidia kupunguza hewa ya kaboni kupitia uoto na husaidia kupooza udongo na hewa. Tutunze mazingira ili mifumo ikolojia iweze kuwa endelevu kwa manufaa yetu na viumbe hai wengine.


**TUNZA MAZINGIRA**

## Kurunzi ya Mazingira yetu




Chanzo kikubwa cha uharibifu wa ardhi oevu ni shughuli za kibinadamu zinazofanyika ndani ya maeneo oevu kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi. Hivyo epuka shughuli za kibinadamu katika maeneo oevu ili kuyalinda kwa maendeleo endelevu ya mazingira.

## Kurunzi ya Mazingira yetu



Ardhi oevu ni rasilimali muhimu inayochangia maendeleo ya Nchi kwani tunapata maji kwa ajili ya kuzalisha nishati ya umeme, kilimo na shughuli za maendeleo. Hivyo tutunze na kulinda ardhi oevu kwa mustakabali wa uchumi wetu.

## Kurunzi ya Mazingira yetu



Ardhi oevu husaidia kuchuja maji yanayokusanyika wakati wa mvua nyingi na kudhibiti mafuriko, lakini pia husaidia kuchuja uchafu na sumu kwenye maji. Linda ardhi oevu kwa mstakabali wa maendeleo endelevu ya Mazingira.

## Kurunzi ya Mazingira yetu



Faida ya ardhi oevu ni vyanzo vikuu vya maji , hutumika katika shughuli za kiutamaduni na utalii, hufyonza hewa ukaa na methane kwenye anga na ni makazi ya viumbe hai. Hivyo tutunze ardhi oevu kwa ustawi wetu sote.

## Kurunzi ya Mazingira yetu



Ardhi oevu ni maeneo ambayo kwa msimu wote wa mwaka huwa na uoto na unyevunyevu au chepechepe. Maeneo haya yana umuhimu katika suala zima la uhifadhi wa mazigira. Pia maeneo haya yana mchango mkubwa katika kuongeza uchumi wa Nchi. Hivyo ni muhimu kulinda ardhi oevu.

## KAULI YA MAZINGIRA YETU




" Athari za mabadiliko ya tabianchi kama mvua kunyesha kupita wastani husababisha janga la mafuriko linalohamisha tope, vifusi na kupeleka sehemu isiyo rasmi hali inayoleta uharibifu wa mazingira. Ni wajibu wa kila mmoja kupanda miti ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**TUNZA MAZINGIRA**


## KAULI YA MAZINGIRA YETU



" Mifumo ya ikolojia ni muhimu kwani huchochea mzunguko wa maji, husaidia kutengeneza rutuba katika udongo, hudhibiti majanga kama mafuriko, hutumika kama makazi ya viumbe hai, maeneo ya kujifunzia na kivutio cha utalii. Tutunze mazingira ili mifumo ikolojia iweze kuwa endelevu kwa manufaa yetu na viumbe hai wengine.

**TUNZA MAZINGIRA**


## KAULI YA MAZINGIRA YETU



" Mifumo ya ikolojia ni muhimu kwani huchochea mzunguko wa maji, husaidia kutengeneza rutuba katika udongo, hudhibiti majanga kama mafuriko, hutumika kama makazi ya viumbe hai, maeneo ya kujifunzia na kivutio cha utalii. Tutunze mazingira ili mifumo ikolojia iweze kuwa endelevu kwa manufaa yetu na viumbe hai wengine.

**TUNZA MAZINGIRA**

## KAULI YA MAZINGIRA YETU



" Mifumo ya ikolojia (Ecosystem) ni mifumo ya kibaiolojia inayoundwa na jamii za viumbe hai (biodiversity) vinavyoingiliana na mazingira asilia wanamoishi kama vile mifumo ya ikolojia ya majini, ardhi, milima, na misitu. Tutunze mazingira ili mifumo ikolojia iweze kuwa endelevu kwa manufaa ya viumbe hai wengine.

**TUNZA MAZINGIRA**

## KAULI YA MAZINGIRA YETU



" Athari za mabadiliko ya tabianchi kama kuvuma kwa upepo mkali huleta athari za miti kuanguka, nyumba kuezuliwa, na kupotea kwa makazi ya wanyama na binadamu. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja kupanda miti katika maeneo yanayotuzunguka ili tuweze kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**TUNZA MAZINGIRA**

## KAULI YA MAZINGIRA YETU



" Athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kama mvua kupita wastani husababisha janga la mafuriko na kuathiri shughuli za kilimo, miundombinu ya barabara, maji, umeme na kupotea kwa baadhi ya viumbe hai muhimu katika mazingira. Ni wajibu wa kila mmoja kupanda miti ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**TUNZA MAZINGIRA**

## Kauli ya Mazingira yetu

JUMATANO 12 JULAI, 2023



Namba 009

Kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) humuwezesha mwekezaji kupata vibali mbalimbali vinavyohusiana na mradi wake, kukubaliwa kwa mradi wake na jamii (social license) na kuepusha migogoro baina ya jamii na mwekezaji. Hivyo ni muhimu kusajili mradi wako sasa.

*Wasiliana nasi;*
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**
Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 296 0098, +255 713 608 930
Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu

Namba ya Bure: **0800110116**
@nemctanzania
NemcTVTanzania
www.nemc.or.tz
@nemctanzania